


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**MUHTASARI WA RIPOTI YA TUME YA KUANGALIA JINSI YA KUBORESHA
TAASISI ZA HAKI JINAI NCHINI**

JULAI, 2023

DODOMA.

YALIYOMO

1.0	UTANGULIZI.....	1
2.0	MAPENDEKEZO YA JUMLA.....	2
2.1	Kubaini na Kuzuia Uhalifu.....	2
2.2	Ukamataji wa Watuhumiwa.....	3
2.2.1	Matumizi Mabaya ya Madaraka.....	4
2.2.2	Matumizi ya Sheria za Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.....	7
2.2.3	Matamko ya Viongozi wa Kisiasa (Mawaziri na Viongozi Wengine wa Serikali).....	8
2.3	Upelelezi na Uchunguzi.....	9
2.4	Makubaliano ya Kukiri Kosa.....	12
2.5	Ulinzi na Usalama wa Watoa Taarifa na Mashahidi.....	14
2.6	Matumizi ya <i>Nolle Prosequi</i>	15
2.7	Dhamana.....	16
2.8	Utitiri wa Vyombo Vyenye Taswira ya Kijeshi.....	17
2.9	Utunzaji wa Vielelezo.....	19
2.10	Upelelezi Binafsi.....	20
2.11	Mwenendo Kabidhi (<i>Committal Proceedings</i>).....	22
2.12	Usikilizwaji wa Awali (<i>Preliminary Hearing</i>).....	23
2.13	Malipo ya Mafao ya Mkupuo ya Kustaafu.....	24
2.14	Utaratibu wa Ajira Katika Jeshi la Polisi na Magereza.....	25
2.15	Maadili na Rushwa.....	26
2.16	Wenye Mahitaji Maalumu Katika Mfumo Wa Haki Jinai.....	27
2.17	Mfuko wa Kufidia Waathirika wa Uhalifu.....	27
2.18	Adhabu ya Kifungo cha Maisha.....	28
2.19	Adhabu ya Kifo.....	29
2.20	Matumizi ya TEHAMA Katika Upelelezi na Uendeshaji wa Mashtaka.....	30
3.0	MAPENDEKEZO MAHUSUSI KWA TAASISI.....	31
3.1	Jeshi la Polisi.....	31
3.1.1	Taswira ya Jeshi la Polisi.....	31
3.1.2	Matumizi ya Amri Kuu za Jeshi la Polisi (PGO).....	32
3.1.3	Usimamizi wa Usalama Barabarani.....	33
3.1.4	Uwajibikaji na Usimamizi Huru wa Jeshi la Polisi.....	34
3.2	Jeshi la Magereza.....	35
3.2.1	Taswira ya Jeshi la Magereza.....	35
3.3	Huduma za Wafungwa na Mahabusu Gerezani.....	36
3.4	Huduma ya Ustawi wa Jamii.....	39
3.5	Idara ya Uangalizi.....	40

3.6	Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.....	40
3.7	Mahakama ya Tanzania	41
3.8	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB)	42
3.9	Ofisi ya Taifa ya Mashtaka	43
3.10	Changamoto za Ujumla za Taasisi za Haki Jinai.....	44
4.0	MASUALA MAHSUSI YA TANZANIA - ZANZIBAR.....	45
4.1	Msamaha wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wanafunzi waliofungwa Tanzania Zanzibar	46
4.2	Vikao vya Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....	47
4.3	Udhibiti wa Makosa ya Rushwa na Dawa za Kulevya Zanzibar	47
4.4	Ushirikiano wa Jeshi la Polisi, Kikosi cha Wanamaji na Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM).....	49
4.5	Chuo cha Mafunzo.....	49

1.0 UTANGULIZI

Tarehe 31 Januari, 2023, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, alizindua Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini chini ya Mwenyekiti Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, Makamu Mwenyekiti Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Balozi Ombeni Yohana Sefue na Wajumbe tisa pamoja na Sekretarieti yake.

Lengo la Mheshimiwa Rais katika kuunda Tume hii ni kupata ushauri na mapendekezo juu ya namna bora ya kuboresha mfumo na utendaji kazi wa taasisi zinazohusika na Haki Jinai. Mapendekezo ya Tume yaliyomo yanatarajiwa kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu utendaji katika taasisi za Haki Jinai na mfumo wa utoaji haki nchini kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na haki za raia.

Tume imebaini kuwa yapo matatizo na changamoto nyingi katika mnyororo wa Haki Jinai, tangu kwenye kuzuia uhalifu; kubaini uhalifu unapotendeka na taarifa kutolewa Polisi; uchunguzi na namna ukamataji wa watuhumiwa unavyofanyika; mashtaka yanapoandaliwa; shauri linapoendeshwa na hukumu kutolewa mahakamani; waliohukumiwa wanapokwenda kufungwa magerezani; na maisha ya wafungwa waliomaliza vifungo vyao wanaporejea uraiani.

Mawanda ya muhtasari huu wa Ripoti ya Tume ni kuonesha ukubwa wa changamoto na namna zinavyoathiri mfumo na utendaji wa taasisi za Haki Jinai katika mnyororo huo. Vilevile, muhtasari huu unawasilisha mapendekezo ya Tume kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kufikia malengo ya Mheshimiwa Rais ya kurekebisha hali hiyo na kukidhi kiu na matarajio ya wananchi kufuatia kuundwa kwa Tume.

Mapendekezo yaliyotolewa ni matokeo ya utafiti na majadiliano ya kina na viongozi wakuu wastaafu, viongozi wastaafu na waliopo madarakani wa taasisi zinazohusika na Haki Jinai, watendaji na watumishi katika taasisi hizo, wadau mbalimbali, vyama vya siasa, viongozi wa dini, waathirika wa mfumo wa Haki Jinai uliopo, vyama vya

kitaaluma, vyama vya wafanyabiashara, uzoefu wa nchi nyingine na wananchi waliofikiwa katika maeneo yao.

Ni matumaini ya Tume kuwa, matokeo ya uchambuzi uliofanyika yatasaidia Serikali kufanya mabadiliko makubwa ili lengo la Mheshimiwa Rais kuunda Tume hii lifikiwe.

2.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA

2.1 Kubaini na Kuzuia Uhalifu

Tume imebaini kuwa hakuna mkakati mahususi wa kitaifa wa kubaini na kuzuia uhalifu ambao, pamoja na mambo mengine, ungeainisha majukumu ya taasisi mbalimbali pamoja na vyombo vya utekelezaji na jamii kwa ujumla. Vilevile, imebainika kuwa vyombo vya utekelezaji sheria vimejikita zaidi katika ukamataji baada ya uhalifu kutokea na sio kubaini na kuzuia uhalifu usitokee. Mbali na ukosefu wa mkakati, upo pia upungufu wa vitendea kazi.

Tume inapendekeza:

- (i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na wadau wengine wa Haki Jinai waandae na kusimamia utekelezaji wa Mkakati Mahususi wa Kubaini na Kuzuia Uhalifu "*Crime Detection and Prevention Strategy*" ikiwemo uhalifu wa majini na mitandaoni.
- (ii) Mfumo wa nyumba kumi uhuishwe kisheria na kutambulika rasmi katika mfumo wa Serikali za Mitaa ili kurahisisha wananchi kutambuana kwa lengo la kuwezesha mkakati wa kuzuia uhalifu kuwa endelevu;

- (iii) Mifumo ya huduma za kijamii na kibiashara zifungamanishwe na mifumo ya utambuzi na usajili (anuani za makazi, RITA, Ardhi na NIDA) ili kila mwananchi awe na namba moja ya utambuzi;
- (iv) Serikali ichukue hatua za kupunguza uchumi wa fedha taslimu (*cash-based economy*) ikiwemo kuondoa vikwazo vilivyopo kwenye mifumo ya malipo na uhamishaji pesa kimtandao;
- (v) Mifumo ya kushirikisha jamii katika kuzuia uhalifu kama vile mfumo wa Polisi Jamii na TAKUKURU - Rafiki iimarishwe na wahusika wapewe mafunzo ya msingi kuhusu majukumu yao na watakiwe kutekeleza kazi zao kwa kuheshimu sheria na haki za binadamu;
- (vi) Serikali ihamasishe na kuwekeza kwa kushirikiana na sekta binafsi, kwenye matumizi ya *CCTV camera* na TEHAMA ili zitumike kwa kiwango kikubwa katika kuzuia na kubaini uhalifu na wahalifu; na
- (vii) Elimu itolewe kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuzuia vitendo vya uhalifu.

2.2 Ukamataji wa Watuhumiwa

Imebainika kuwa, vyombo vyenye mamlaka ya kukamata, mara nyingi hutumia nguvu kubwa kupita kiasi na kusababisha mateso kwa watuhumiwa. Uwepo wa taasisi nyingi zenye mamlaka ya kukamata pia umelalamikiwa na wananchi kuwa inakuwa vigumu kutambua taasisi iliyomkamata ndugu yao na mahali alipohifadhiwa. Aidha, uwepo wa vyombo vingi vya ukamataji na vyenye mahabusu umetafsiriwa na jamii kuwa ni sababu mojawapo ya watu waliokamatwa kupotea wakiwa mikononi mwa vyombo vya dola.

Tume inapendekeza:

- (i) Mamlaka ya kukamata waliyonayo mamlaka za usimamizi (*regulatory bodies*) yatekelezwe kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi;

- (ii) Taasisi nyingine zenye mamlaka ya kukamata zifanye ukamataji kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi;
- (iii) Mahabusu za Jeshi la Polisi ndizo pekee zitumike kuhifadhi watuhumiwa wa makosa ya jinai; na
- (iv) Mamlaka husika zichukue hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wanaokiuka taratibu za kazi ya ukamataji na uhifadhi wa watuhumiwa.

2.2.1 Matumizi Mabaya ya Madaraka

Vyombo vilivyo na mamlaka ya kukamata vinapaswa kutumia mamlaka hayo kwa ajili ya kuzuia na kupambana na uhalifu. Hata hivyo, wakati mwingine, vyombo tajwa vimekuwa vikitumia vibaya mamlaka yake ya ukamataji na hivyo kusababisha bughudha na kero kwa wananchi. Mathalan, kukamata watu bila sababu na kukamata watu kwa makosa ya madai. Kutokana na kuwekwa mahabusu bila sababu za msingi, Mchungaji Mtikila alifungua na kushinda shauri dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (*Mchungaji Christopher Mtikila dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali*) kutokana na kuwekwa mahabusu bila sababu za msingi (*false imprisonment*).¹ Aidha, katika shauri la *Mary Peter Otaru dhidi ya Onesmo Buswelo na Wenzake*,² mlalamikaji aliwekwa mahabusu kwa siku tano na Mkuu wa Wilaya ya Siha kutokana na shauri la madai. Kwa kuwa Mkuu wa Wilaya hakuzingatia sheria katika kutoa amri ya kumweka mahabusu mlalamikaji, Mahakama Kuu iliagiza Serikali kumlipa mlalamikaji fidia ya Shilingi milioni tisini.

Tume imebaini kuwa imejengeka desturi ya baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kutumia Sheria ya Tawala za Mkoa, Sura

¹ [2004] TLR. 172

² Civil Case No.9 of 2020. High Court, Moshi District Registry. (*Unreported*)

ya 97 na Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61 kuminya haki za wananchi kwa masuala mbalimbali bila kuzingatia masharti yaliyowekwa na sheria. Aidha, Tume imebaini kuwa, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamekuwa wakiambatana na Wajumbe wa Kamati za Usalama katika ziara mbalimbali hata zile zisizostahili uwepo wa vyombo hivi.

Tathmini ya Tume imebaini kuwa, kwa sasa viongozi hawa hujitambulisha kama Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama kinyume na Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61 inayowatambua kama Wenyeviti wa Kamati za Usalama za Mikoa au Kamati za Usalama za Wilaya. Vilevile, desturi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuambatana na Kamati za Usalama katika ziara zao inaweza kusababisha hofu kwa wananchi na kuwafanya washindwe kufikisha mawazo na kero zao kwa viongozi hao. Pia, kwa viongozi hao kuambatana na Kamati za Usalama kunasimamisha baadhi ya majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na Wajumbe wa Kamati za Usalama kwa nafasi zao. Mathalan, wakuu wa vyombo vinavyohusika wanakosa muda wa kutosha wa kutekeleza majukumu yao ya msingi na mara nyingi hutumia vyombo vya usafiri vinavyohitajika katika utekelezaji wa majukumu mengine ya chombo kinachohusika. Aidha, desturi hii inaiongezea Serikali gharama kubwa ya matumizi ya fedha za umma.

Tume inapendekeza:

- (i) Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura ya 97 irekebishwe ili kuondoa mamlaka ya ukamataji waliyonayo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wengine kwa nafasi zao na badala yake viongozi hao wafuate utaratibu uliopo katika Sheria ya

Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura 20 ambao unaruhusu mtu yeyote kumkamata mtu anayefanya kosa mbele yake;

- (ii) Endapo ni muhimu kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuendelea kuwa na mamlaka ya ukamataji, viongozi hao waelekezwe kuwa wanapotekeleza mamlaka hayo kupitia vifungu vya 7 na 15 vya Sheria ya Tawala za Mikao, Sura ya 97 mtawalia, wazingatie masharti yote yaliyoelekezwa kupitia vifungu tajwa. Baadhi ya masharti hayo ni: kosa liwe linatendeka mbele yake, liwe kosa la jinai ambalo mtu anaweza kushtakiwa, kosa litakalokuwa limetendwa liwe limesababisha kuvunjika kwa amani na utulivu na hakuna namna ya kulizuia kutendeka, ni lazima Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, mara baada ya mtuhumiwa kukamatwa, amwandikie hakimku kueleza sababu zilizosababisha mtuhumiwa kukamatwa.
- (iii) Mara baada ya maelekezo hayo ya kuzingatia matakwa ya sheria kutolewa, kiongozi yeyote atakayeyakiuka itabidi achukuliwe hatua kali, na iwapo mwathirika wa maagizo yake atafungua shauri Mahakamani, basi huyo kiongozi awajibike yeye mwenyewe na Serikali isiwe sehemu ya shauri hilo.
- (iv) Serikali itoe maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusitisha utaratibu wa kuambatana na Wajumbe wa Kamati za Usalama pasipo kuwa na ulazima na pia waache kujitambulisha kama wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama;
- (v) Askari polisi au watendaji wengine wa vyombo vyenye mamlaka ya ukamataji wanaotumia vibaya mamlaka hayo wachukuliwe hatua za kinidhamu; na
- (vi) Wananchi wapewe elimu ili waweze kutambua haki zao ndani ya Mfumo wa Haki Jinai.

2.2.2 Matumizi ya Sheria za Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Serikali za mitaa ni sehemu ya Serikali iliyo karibu na wananchi katika ngazi ya msingi kwa lengo la kuwashirikisha katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo kwenye maeneo yao.

Tume ilipokea maoni ya wadau kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa (halmashauri) kuanzisha makosa ya jinai kupitia sheria ndogo (*by-laws*) na kupendekeza mamlaka hizo zipunguziwe nguvu za kijinai. Aidha, Tume ilichambua sheria za serikali za mitaa ili kubaini vifungu vinavyoanzisha makosa ya jinai na kutoa mamlaka ya ukamataji kwa maafisa wa serikali za mitaa. Hivyo, Tume ilibaini yafuatayo:-

(a) Mamlaka ya Kipolisi ya Wakurugenzi na Maafisa wa Halmashauri

Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, inawapa Wakurugenzi wa Miji majukumu ya kushughulikia uhalifu. Kifungu cha 74 (1)(a) na (b) cha Sheria hiyo kinampa mamlaka Mkurugenzi wa Mji anapopata taarifa kuwa mtu yeyote amefanya kosa la jinai kuagiza mtu huyo kukamatwa na kufikishwa Mahakamani. Aidha, Mkurugenzi anapotekeleza majukumu ya ukamataji atakuwa na mamlaka kama aliyonayo afisa wa polisi na atatekeleza mamlaka na kazi ya ukamataji kama ambavyo sheria imewapa mamlaka hayo maafisa wa polisi.

(b) Mamlaka ya Kukamata na Kuzuia

Kifungu cha 100 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 kinampa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji au Mtendaji wa Kata mamlaka ya kumkamata mtu yeyote anayetenda kosa kinyume na

sheria ndogo za halmashauri³ endapo atafanya hivyo mbele yake. Aidha, sheria inampa mamlaka Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya kutoa kibali cha maafisa hao kumuweka kizuizini mtuhumiwa aliyekamatwa kwa muda mpaka atakapofikishwa mahakamani.

Tume inapendekeza:

- (i) Mamlaka ya kipolisi waliyonayo Wakurugenzi wa Halmashauri, yaondolewe kwenye sheria, badala yake mamlaka hayo yatekelezwe na Jeshi la Polisi.
- (ii) Mamlaka aliyonayo Mkurugenzi na Afisa Mtendaji Kata kukamata na kuweka kizuizini watuhumiwa yaondolewe; na
- (iii) Jeshi la Polisi lifikishe huduma zake katika kata zote.

2.2.3 Matamko ya Viongozi wa Kisiasa (Mawaziri na Viongozi Wengine wa Serikali)

Wakati mwingine matamko ya viongozi wa kisiasa na wa Serikali yamekuwa kwa namna moja au nyingine yakiathiri haki za watu. Hali hii, imezua malalamiko ya wananchi wanaohoji mipaka na mamlaka ya viongozi wa kisiasa hasa Mawaziri na Watumishi wa Serikali kujipa mamlaka yasiyotokana na sheria na kuamuru vyombo vya dola kukamata na kuwaweka ndani wananchi. Malalamiko haya ya wananchi ni ya msingi na ni muhimu yafanyiwe kazi ili kuimarisha misingi ya utawala bora na utawala wa Sheria.

Tume inapendekeza:

- (i) Mamlaka ya uteuzi wa viongozi ielekeze viongozi wote wasio na mamlaka mahsusi ya kisheria ya ukamataji kuzingatia taratibu zilizowekwa na Sheria katika kutoa amri za ukamataji; na

³ Mamlaka haya pia yametolewa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo, Afisa tarafa na Mtendaji Kata chini ya kifungu cha 184 cha Sheria ya Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287.

- (ii) Mara baada ya maelekezo hayo kutolewa na kiongozi yeyote kukiuka maelekezo hayo, kiongozi huyo awajibike yeye mwenyewe na Serikali isiwe sehemu ya shauri litakalotokana na ukiukwaji huo.

2.3 Upelelezi na Uchunguzi

Ubora wa upelelezi na uchunguzi ndio msingi wa haki kupatikana kwa wakati. Hivyo, masuala ya uwezo na weledi wa wapelelezi, vitendea kazi, uadilifu, uwajibikaji na ufanisi ni masuala ya msingi katika kuboresha mfumo na utendaji wa taasisi za Haki Jinai.

Kutotenganishwa kwa Idara ya Upelelezi na shughuli nyingine za Jeshi la Polisi kumesababisha ucheleweshaji wa upelelezi, ukosefu wa ubobevu (*specilization*) na ufanisi mdogo katika upelelezi. Jambo hilo limechangiwa na wapelelezi walio chini ya Jeshi la Polisi, wakati mwingine, kupangiwa shughuli nyingine ambazo hazihusiani na upelelezi.

Aidha, Idara ya Upelelezi hutegemea bajeti ya Jeshi la Polisi ambalo lina vipaumbele vingi hivyo kusababisha idara hii kushindwa kuwa na wataalamu wa kutosha kama vile wachunguzi wa vifo, wahasibu, wahandisi, na wataalamu wa TEHAMA; pamoja na kushindwa kuwa na vitendea kazi vya kisasa kwa ajili ya upelelezi, kutoa mafunzo kwa wapelelezi na kuhuisha mitaala ili iendane na wakati na mazingira ya sasa.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), katika utekelezaji wa majukumu yake ya uchunguzi, imekuwa ikikumbana na changamoto mbalimbali, mathalani; baadhi ya wachunguzi wa Taasisi kujihusisha na rushwa, ukosefu wa wachunguzi wabobevu wenye weledi wa kutosha kuhusu masuala ya rushwa, kukosekana kwa mafunzo ya uchunguzi, ufinyu wa bajeti ya uchunguzi na kutokuwa na maabara rasmi iliyorasimishwa katika uchunguzi wa rushwa za kimtandao. Changamoto nyingine ni uchache wa vitendea kazi, kukosa ushirikiano kutoka kwa

wananchi pale chunguzi za matukio mbalimbali ya rushwa zinapochunguzwa na mashahidi kutokutoa ushirikiano pindi mashtaka yanapofikishwa mahakamani.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (*DCEA*), kama ilivyo kwa Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, hutekeleza majukumu ya upelelezi wa makosa ya dawa za kulevya. Pamoja na utekelezaji wa majukumu hayo, Mamlaka inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazosababisha vita dhidi ya dawa za kulevya kudhoofika kwa kuwa Mamlaka si chombo cha Muungano na hivyo udhibiti wa biashara hii kuwa mgumu. Mafanikio katika vita hii yanahitaji nguvu ya pamoja ya pande mbili za Muungano zenye mtazamo sawa wa kupambana na dawa za kulevya. Aidha, Mamlaka haijaenea nchi nzima; kwa sasa ipo katika ngazi ya Kanda tu, hali inayosababisha muingiliano wa majukumu ya kipelelezi na taasisi nyingine za upelelezi. Mathalan, Kitengo cha Udhibiti wa Dawa za Kulevya (*Anti - Drug Unit -ADU*) cha Jeshi la Polisi; Mamlaka kutokuwa na wapelelezi wabobevu wenye weledi; na kutokuwepo kwa miundombinu na vitendea kazi toshelevu vya upelelezi.

Hali ya kuwa na taasisi nyingi zinazojihusisha na upelelezi wa makosa ya jinai kama ilivyo sasa imesababisha athari zifuatazo:-

Kwanza, migongano baina ya vyombo pelelezi kwa kutoelewa mipaka ya majukumu kati ya taasisi moja na nyingine kutokana na makosa ya jinai kuwa na muunganiko katika utendaji wake (mathalani makosa ya dawa za kulevya, makosa ya rushwa na makosa ya ujangili yana mfungamano na utakasishaji fedha haramu) ambapo makosa hayo yanapelelezwa na taasisi tofauti. Hali hii, imesababisha baadhi ya taasisi za kiupelelezi kufanya majukumu yasiyo na mamlaka nayo kisheria na hivyo upelelezi kutofanyika kwa ukamilifu. Hali hii inaathiri eneo muhimu la uwajibikaji, pale wahusika wanapokuwa wengi.

Pili, ongezeko la gharama kwa Serikali kutokana na mgawanyo wa rasilimaliwatu na fedha pamoja na vitendea kazi kama vile maabara za kisasa kwa ajili ya uchunguzi, boti, magari, ofisi, samani, vyumba vya mahabusu na taasisi za mafunzo ili kutosheleza mahitaji ya taasisi hizo nchi nzima.

Tatu, taasisi tajwa hazina mfumo wa usimamizi na udhibiti wa matumizi ya mamlaka yake hivyo kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi.

Nne, uwepo wa taasisi nyingi zinazohusiana na upelelezi umesababisha changamoto za uratibu na utunzaji wa takwimu za uhalifu.

Tano, mbali na Jeshi la Polisi, taasisi zinazotekeleza majukumu ya upelelezi hazijaenea maeneo yote nchini na gharama kubwa itahitajika ili kuziwezesha taasisi hizo kufika maeneo yote.

Sita, vikosi kazi vinavyoundwa na taasisi za upelelezi na uchunguzi ili kushughulikia kwa dharura jinai vimelalamikiwa kwa kukosa ufanisi, uwajibikaji na muendelezo.

Kwa kuzingatia uzoefu wa nchi nyingine, Tume ina maoni kuwa uwajibikaji na ufanisi unaongezeka zaidi endapo taasisi ya upelelezi na uchunguzi itakuwa moja na itajitegemea.

Tume inapendekeza:

- (i) Ili kuweka usimamizi na mfumo madhubuti wa upelelezi na uchunguzi, Serikali iunganishe nguvu ya upelelezi na uchunguzi iliyopo sasa katika taasisi mbalimbali za upelelezi wa makosa ya jinai na kuanzisha Mamlaka mpya na huru ya upelelezi inayojitegemea itakayojulikana kama Ofisi ya Taifa ya Upelelezi (OTU) (*National Bureau of Investigation*) ambayo itakuwa na jukumu la kupeleleza makosa yote makubwa ya jinai. Pia inapendekezwa mamlaka mpya iwe na bajeti inayojitegemea, uwezo wa kuajiri watumishi, kuwa na chuo bora cha mafunzo na maabara moja ya kisasa kwa ajili ya uchunguzi wa

kisayansi, mifumo ya TEHAMA na kuimarisha ubobevu (*specialization*) wa wapelelezi. Aidha, muundo, majukumu na mipaka ya utendaji itabainishwa katika sheria.

- (ii) Sheria iweke ukomo wa muda wa upelelezi kwa makosa yanayosikilizwa na Mahakama Kuu.

2.4 Makubaliano ya Kukiri Kosa

Makubaliano ya kukiri makosa ya jinai (*plea bargaining*) ni utaratibu wa kumaliza kesi za jinai mahakamani kwa njia ya makubaliano ambapo mshtakiwa anakubali kukiri kosa analoshtakiwa nalo au kosa dogo miongoni mwa makosa aliyoshtakiwa nayo au kwa makubaliano na mwendesha mashtaka kumshtaki kwa kosa dogo au kosa lenye adhabu ndogo. Utaratibu wa makubaliano ya kukiri kosa unafanyika katika nchi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Marekani, Afrika Kusini, India, Ufilipino, Kenya na Zambia.

Utaratibu wa makubaliano ya kukiri kosa nchini unasimamiwa na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura 20; *The Criminal Procedure (Plea Bargaining Agreement) Rules, G.N No. 180 of 2021*; Notisi ya Ugatuzi wa Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Mwaka 2022⁴ na Mwongozo wa Mkurugenzi wa Mashtaka wa Makubaliano ya Kukiri Kosa wa Mwaka 2022.⁵ Utaratibu wa kukiri kosa unahusisha hatua kuu tatu ambazo ni: kuwasilisha mahakamani taarifa ya kusudio la kuingia makubaliano ya kukiri kosa (*notice*); marekebisho ya hati ya mashtaka; na kusainiwa na kuusajili mahakamani mkataba wa kukiri kosa (*plea bargaining agreement*).

Tume ilipokea maoni ya wadau kuhusu utekelezaji wa utaratibu wa kukiri kosa ambapo ilibainishwa kuwa kulikuwepo na uchelewaji wa mashauri kumalizika kwa utaratibu huo kutokana na ridhaa ya *DPP* kutopatikana kwa wakati; washtakiwa kulazimishwa kuingia mikataba ya kukiri makosa bila

⁴ Tangazo la Serikali Na.467/2022

⁵ Wasilisho la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa Tume ya Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai 2023 ukurasa wa 219 hadi 259

hiari; na kutokuwepo kwa uwazi kwa kuwa mashauri ya kukiri kosa nchi nzima kushughulikiwa na DPP na timu maalumu ya maafisa wanne pekee.

Tume ilipitia majalada ya mashauri yaliyomalizwa kwa utaratibu tajwa na kufanya uchambuzi wa Sheria inayosimamia utaratibu huo na kubaini kuwa, baadhi ya washitakiwa waliokiri makosa hawakumaliza kulipa kiwango cha fedha kilichopo kwenye mikataba, utaratibu wa kukiri makosa ulifanyika katika awamu kuu tatu; awamu ya kwanza ni mashauri kuanzia mwaka 2019 hadi Januari, 2021 baada ya marekebisho ya CPA na kabla ya kutungwa kwa *The Criminal Procedure (Plea Bargaining Agreement) Rules, G.N No. 180 of 2021* (Kanuni za Jaji Mkuu); awamu ya pili ni mashauri kuanzia Februari mwaka 2021 hadi Mei, 2022 baada ya kutungwa Kanuni za Jaji Mkuu na kabla ya DPP kugatua madaraka yake katika Mikoa na Wilaya; na awamu ya tatu ni mashauri yaliyofanyika Juni 2022 mpaka sasa baada ya DPP kugatua madaraka yake katika mikoa na wilaya.

Ilibainika zaidi kuwa malalamiko yaliyotolewa na wadau yalitokana na mfumo wa kisheria uliokuwepo hasa katika awamu ya kwanza na ya pili ya utekelezaji wa plea bargaining ambapo Sheria ilianza kutekelezwa bila kuwepo kwa Kanuni zinazoelekeza utaratibu mahsusi wa kufuatwa na mamlaka ya DPP kutogatuliwa mikoani na kwa maafisa wengine. Hata hivyo, baada ya Kanuni za Jaji Mkuu kutungwa mwaka 2021, na mamlaka ya DPP kugatuliwa katika ngazi za mikoa na wilaya mwaka 2022 upungufu wa kimfumo ulioibuliwa ulirekebishwa.⁶

Tume inapendekeza:

- (i) Elimu zaidi itolewe kwa wananchi na wadau muhimu kuhusu utaratibu wa *plea bargaining*;

⁶ Uchambuzi wa kina wa utekelezaji wa utaratibu wa kukiri kosa upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji

- (ii) Malalamiko ya washtakiwa kulazimishwa kuingia katika makubalino ya kukiri kosa yashughulikiwe kwa njia ya mahakama kwa mujibu wa sheria ili haki itendeke kwa pande zote;
- (iii) Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itunze kumbukumbu za majadiliano ya makubaliano ya kukiri kosa; na
- (iv) Iundwe timu maalumu ya kuchunguza utata katika baadhi ya mali zilizotaifishwa katika utaratibu wa vikosi kazi na mashauri ya kukiri kosa ili kuishauri Serikali ipasavyo.

2.5 Ulinzi na Usalama wa Watoa Taarifa na Mashahidi

Sheria ya Ulinzi wa Watoa Taarifa na Mashahidi, Sura ya 446, inalenga kutoa ulinzi kwa watoa taarifa na mashahidi. Hata hivyo, Sheria hiyo haijabainisha taasisi mahsusi ya kusimamia na kuratibu ulinzi na usalama wa watoa taarifa na mashahidi. Mathalan, katika kifungu cha 11 cha Sheria hii inabainisha kuwa, mamlaka yenye jukumu la kumlinda mtoa taarifa na shahidi ikiona kuwa upo uwezekano wa maisha au mali za mtu huyo kuwa hatarini itawasilisha suala hilo kwa taasisi yenye mamlaka ya kumlinda mtoa taarifa na shahidi huyo. Taasisi hiyo yenye mamlaka ya kumlinda mtoa taarifa na shahidi haijabainishwa katika Sheria hiyo.

Tume inapendekeza:

- (i) Sheria ya Ulinzi wa Watoa Taarifa na Mashahidi ifanyiwe marekebisho na kubainisha taasisi mahsusi ya kuratibu ulinzi wa mashahidi na watoa taarifa nchini ili kuimarisha ulinzi wao; na
- (ii) Taasisi husika iwe na bajeti ya kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake.

2.6 Matumizi ya *Nolle Prosequi*

Tume imepokea malalamiko ya wadau kuhusiana na matumizi ya *nolle prosequi* ambapo, baadhi ya watuhumiwa waliofutiwa mashtaka, hukamatwa tena na kushtakiwa kwa makosa sawa na yale yaliyofutwa.

Tume imebaini kuwa, Tume ya Mapitio ya Mfumo wa Mahakama ya Mwaka 1977 maarufu kama *Tume ya Msekwa* ilieleza dhahiri kuwa *nolle prosequi* haimalizi shauri. Hivyo, mtuhumiwa anaweza kukamatwa na kushtakiwa tena kwa kosa sawa na lile alilofutiwa. Aidha, ili kulinda haki ya mtuhumiwa, zimefanyika jitihada mbalimbali za kuzuia matumizi mabaya ya mamlaka ya *nolle prosequi* nchini. Mathalan, mwaka 2022 kifungu cha 91(3) cha CPA kiliongezwa ili kuzuia mtuhumiwa kukamatwa na kushtakiwa tena ikiwa upelelezi haujakamilika. Kwa kuwa Sheria imerekebishwa hivi karibuni, Tume imebaini kuwa, hakuna uelewa wa kuridhisha kuhusu matumizi ya kifungu cha 91(3) cha CPA ambacho kinaweka sharti kuwa mtuhumiwa akishtakiwa tena baada ya kufutiwa kosa, ni sharti pawepo ushahidi wa kutosha na usikilizaji wa shauri uanze siku hiyo ya kusomewa shauri upya.

Tume inapendekeza:

- (i) Utaratibu wa *nolle prosequi* uendelee kuwepo kutokana na umuhimu wake katika kulinda maslahi ya umma kwa kumuwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kufuta mashauri ambayo yamekosa uhalali wa kuwepo mahakamani wakati uamuzi huo unafikiwa;
- (ii) Elimu itolewe kwa wadau wote wa Haki Jinai kuhusu maboresho ya mfumo wa *nolle prosequi* yaliyofanyika kufuatia marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai yaliyofanyika na kuweka sharti kuwa, mashauri yasifunguliwe pasipokuwa na ushahidi wa kutosha wa kuwasilisha mahakamani na kuendelea na usikilizwaji;

- (iii) Marekebisho yaliyofanyika yakishindwa kutatua changamoto za matumizi ya mamlaka ya *nolle prosequi*, marekebisho zaidi yafanyike ili *nolle prosequi* iwe inatolewa kwa ridhaa ya mahakama; na
- (iv) Maafisa wa mahakama na waendesha mashtaka watakaoshindwa kuzingatia matakwa ya Sheria chini ya kifungu cha 91(3) cha CPA wachukuliwe hatua za kinidhamu na mamlaka zao za ajira.

2.7 Dhamana

Tume imepokea malalamiko ya wadau mbalimbali kuhusu sheria kutoruhusu dhamana kwa baadhi ya makosa. Hivyo, ilipendekezwa na baadhi ya wadau kuwa, makosa yote nchini yawe na dhamana kama ilivyo kwa nchi nyingine ikiwa ni pamoja na Kenya. Hata hivyo, wadau wengine walipendekeza kuwa makosa makubwa kama vile ugaidi, mauaji, uhaini, ubakaji na ulawiti wa watoto chini ya miaka kumi ndiyo yaondolewe dhamana lakini makosa mengine yote yawe na dhamana. Aidha, tafsiri ya makosa tangulizi (*predicate offence*) ya utakasishaji wa fedha haramu na taratibu za dhamana zilizopo katika Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200, zimeonekana kuchangia washtakiwa wengi kukosa dhamana.

Tume imefanya tathmini ya mapendekezo ya wadau kuhusu makosa yote kuwa na dhamana kama inavyopendekezwa na kujiridhisha kuwa baadhi ya makosa yaliyotajwa katika Kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, hayapaswi kuwa na dhamana kutokana na uzito wa kosa na adhabu yake, uwezekano mkubwa wa mtuhumiwa kuharibu ushahidi au kuingilia upelelezi na wananchi kujichukulia sheria mkononi dhidi ya watuhumiwa na watuhumiwa kuhitaji hifadhi ya kisheria kwa usalama wao wenyewe.

Tume inapendekeza:

- (i) Bila kuathiri masharti ya mikataba ya Kimataifa ambayo Serikali imeingia kuhusu kudhibiti makosa makubwa ya kupangwa na makosa

ya uhujumu uchumi, tafsiri ya makosa tangulizi ya kosa la utakasishaji fedha haramu irekebishwe ili kupunguza washtakiwa wengi kukosa dhamana kutokana na tafsiri hiyo kuwa pana;

- (ii) Jedwali linaloainisha makosa ya uhujumu uchumi katika Sheria ya Udhhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200, lipitiwe upya ili kuweka kigezo cha thamani ya mali au fedha inayohusika na kesi hiyo ili kudhibiti mamlaka na kutathmini endapo makosa yote yaliyobainishwa kwenye jedwali hilo yanapaswa kuendelea kuwa ya uhujumu uchumi;
- (iii) Sheria ya Kudhibiti Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu ya Kupangwa, Sura ya 200, ifanyiwe marekebisho ili maamuzi ya kumnyima dhamana mtuhumiwa yatolewe na mahakama;
- (iv) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20, irekebishwe ili mashauri ya makosa yasiyo na dhamana yaanze kusikilizwa ndani ya muda maalumu utakaowekwa kisheria na ikiwa mashauri hayajaanza kusikilizwa ndani ya muda huo, dhamana itolewe isipokuwa kama mahakama itaona kuna sababu za msingi za kumnyima dhamana mshtakiwa huyo; na
- (v) Itungwe sheria mahususi ya dhamana (*Bail Act*) itakayoainisha mfumo, mamlaka na utaratibu wote wa dhamana ili kuliweka suala la dhamana kwenye sheria moja na kupunguza mamlaka zinazoshughulikia dhamana.

2.8 Utitiri wa Vyombo Vyenye Taswira ya Kijeshi

Uwepo wa vyombo vya Haki Jinai vinavyotekeleza majukumu yake kwa taswira ya kijeshi (*militarisation of criminal justice*), umesababisha: matumizi ya nguvu kupita kiasi dhidi ya watuhumiwa katika ukamataji; upekuzi na mahojiano; ubebaji na matumizi ya silaha za kivita; uvaaji wa vyeo vinavyoshabihiana na vyeo vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

(JWTZ); na taasisi kujilinganisha hadhi na JWTZ. Vyombo hivyo ni pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Uhamiaji na Jeshi Usu la Uhifadhi.

Utitiri wa vyombo vyenye taswira ya kijeshi umesababisha taasisi zenye sura ya kijeshi kuwa nyingi, taasisi za Haki Jinai kukosa ushirikiano kutoka kwa wananchi kutokana na kuwepo kwa malalamiko ya wananchi juu ya kunyanyaswa na kuteswa na taasisi zenye taswira ya kijeshi, na kuwepo kwa uwezekano wa kusambaa kwa silaha, suala linaloweza kutishia amani nchini. Aidha, awali shughuli za Zimamoto zilikuwa Halmashauri za Wilaya hivyo zikigatuliwa na kwenda Serikali za Mitaa zitafanya huduma za zimamoto ziwe karibu na wananchi. Vilevile, ugatuzi huo utasaidia kufungamanisha shughuli za zimamoto na uokoaji na shughuli za mipango miji ambazo hutekelezwa na Serikali za Mitaa.

Tume inapendekeza:

- (i) Utaratibu wa kuanzisha taasisi zenye taswira ya kijeshi usitishwe;
- (ii) Taasisi ambazo zinatekeleza majukumu ya Haki Jinai au zinazotoa huduma kwa wananchi zenye taswira ya kijeshi, mathalani Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Uhamiaji na Jeshi Usu la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu zirejee katika majukumu yake ya awali ya utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (iii) Huduma za Zimamoto na Uokoaji zirejeshwe na kutekelezwa katika ngazi za halmashauri hasa ikizingatiwa shughuli za zimamoto zina muingiliano mkubwa na shughuli nyingine za halmashauri katika mipango miji; na
- (iv) Mafunzo kwa Askari wa Uhifadhi wa Misitu na Wanyamapori yatolewe na Jeshi la Polisi kwa kuzingatia misingi ya Haki za Binadamu na utawala wa Sheria.

- (v) Wizara ya Maliasili na Utalii iwarejeshe watumishi wote raia katika vyeo vyao vya ajira ya awali na kuwaondolea mavazi na vyeo vya kijeshi isipokuwa mavazi yavaliwe na watumishi walioko kwenye Idara inayohusika na majukumu ya kupambana na ujangili.

2.9 Utunzaji wa Vielelezo

Imebainika kuwa utunzaji wa vielelezo katika baadhi ya vituo vya polisi vilivyotembelewa na Tume hauzingatii ipasavyo miongozo na sheria. Vituo vya Polisi vinakabiliwa na ufinyu wa nafasi ya kuhifadhi vielelezo na hakuna umakini wa kutosha miongoni mwa watendaji katika utunzaji wa vielelezo. Hali hii inachangia Jamhuri kushindwa mashauri mahakamani kwa sababu ya kuharibika kwa vielelezo. Aidha, kuharibika au kupotea kwa vielelezo huisababishia Serikali hasara kwa kulipa fidia pale amri inapotolewa ya kurejesha vielelezo tajwa kwa mmiliki wake.

Tume inapendekeza:

- (i) Serikali iwezeshe Jeshi la Polisi na taasisi nyingine za uchunguzi kuwa na miundombinu ya kisasa na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kuhifadhi, utoaji wa vielelezo mahakamani na uondoshaji wa vielelezo (*disposal*); mathalan, kusomana kwa mfumo wa uchukuaji, upokeaji, uhifadhi, utoaji wa vielelezo mahakamani na uondoshaji wake kati ya Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Mahakama ya Tanzania.
- (ii) Kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika uhifadhi wa vielelezo;
- (iii) Taasisi za uchunguzi na upelelezi zitoe mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji wanaohusika na utunzaji wa vielelezo;
- (iv) Taasisi za Haki Jinai ziweke taratibu na mkakati madhubuti wa kuteketeza vielelezo hatarishi; na
- (v) Watendaji waepuke kukamata vielelezo na kuvichukua bila kupata ushahidi unaoviunganisha na kesi au tuhuma iliyotolewa taarifa.

2.10 Upelelezi Binafsi

Tume imepokea maoni kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa upelelezi binafsi kwa ajili ya kukidhi mahitaji binafsi katika sekta ya upelelezi na uchunguzi. Pamoja na huduma hii kutolewa hapa nchini, Tume imebaini kuwa, ipo changamoto ya uendeshaji wa huduma hii pasipokuwepo na sheria mahususi inayoweka masharti mbalimbali kuhusu upelelezi binafsi. Kwa sasa, zipo kampuni na watu binafsi wanaojihusisha na huduma ya upelelezi binafsi hasa katika taasisi za kifedha, mashirika ya bima na kampuni za mitandao ya simu. Kupitia huduma hizi yapo mafanikio mbalimbali yaliyowezesha kubainika kwa uhalifu, kuwaunganisha ndugu na familia zao, kutatua migogoro ya kijamii hasa ya kifamilia, kibiashara na kisiasa. Hivyo, ni muhimu suala hili likawekewa utaratibu rasmi ili sekta ya upelelezi binafsi iweze kurasimishwa katika mfumo wa kisheria.

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 322, Jeshi la Polisi ndio chombo kikuu cha upelelezi hapa nchini. Aidha, taasisi nyingine zenye mamlaka ya kisheria kufanya upelelezi na uchunguzi ni TAKUKURU chini ya vifungu vya 7(e) na (f) na 10 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevya chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, Sura ya 95.

Tume imefanya uchambuzi wa maoni na mawasilisho ya wadau na kuangalia uzoefu wa nchi nyingine kama vile Australia, Canada, Kenya na Uingereza. Uzoefu huo umebainisha faida mbalimbali za upelelezi binafsi kama vile kusaidia kupata taarifa ambazo ni muhimu zinazohusiana na mashauri ya jinai, kukutana na ndugu waliopotea na kupata taarifa za uhakika za watu unaotarajia kuingia nao katika mkataba (*due diligence*). Pamoja na faida zake, upelelezi binafsi unapaswa kuwekewa masharti mahususi katika utekelezaji wake. Masharti hayo yatajumuishwa: mpelelezi binafsi kutohitaji au kutumia

taarifa za siri za Serikali; kujifanya ni askari polisi; na kutotumia vibaya taarifa binafsi za mtu au kampuni au kuingia kwa jinai (*criminal trespass*) katika maeneo ya watu.

Uzoefu huo umeonesha kuwa, wapelelezi binafsi wanatumika katika Mfumo wa Haki Jinai kwa kuwa wamekuwa ni sehemu ya msaada kwa vyombo chunguzi vya Umma katika kubaini, kuzuia na kupambana na uhalifu. Sifa mojawapo ya mpelelezi binafsi ni ubobevu katika eneo la uchunguzi. Aidha, nafasi ya upelelezi binafsi katika mfumo wa Haki Jinai, inaweza kuangaliwa kwa mtazamo kuwa, watu wengi wanachunguzwa kutokana na vitendo vya jinai lakini hawafikishwi katika mfumo wa Haki Jinai kwani mashauri husika humalizwa kwa maelewano ya pande zinazokinzana.

Kutokana na uzoefu huo, Tume imebaini kuwa ili mfumo wa matumizi ya wapelelezi binafsi uweze kufanya kazi vizuri ni lazima kuwe na mfumo wa kisheria utakaoweka masharti ya watu na sifa za kufanya kazi ya upelelezi binafsi, vigezo vya kupata leseni na sharti la ushirikiano na vyombo vya utekelezaji wa sheria. Nia kubwa ni kuhakikisha haki na faragha zinalindwa. Tume ya Kurekebisha Sheria ya Australia katika taarifa yake kuhusu Sheria ya Faragha na Utekelezaji ilibainisha kuwa wapelelezi binafsi ni tofauti na vyombo vya utekelezaji wa serikali kwa kuwa hawawajibiki moja kwa moja kwa serikali au chombo cha *ombudsman* ambacho kinaweza kuchunguza malalamiko na kutoa fidia kama ambavyo kinafanya kwa vyombo vya serikali. Tume hiyo ilipendekeza umuhimu wa masharti magumu ya leseni ili kusimamia haki ya faragha ya mtu.

Tume inapendekeza:

Itungwe sheria itakayoruhusu na kusimamia upelelezi binafsi ambayo itaanisha mamlaka itakayosimamia na kuratibu upelelezi binafsi, masharti ya usajili, aina ya upelelezi unaoweza kufanywa na wapelelezi binafsi, mipaka ya

upelelezi binafsi, maadili na wajibu wa wapelelezi binafsi kwa Ofisi ya Taifa ya Upelelezi (OTU), Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya kiuchunguzi.

2.11 Mwenendo Kabidhi (*Committal Proceedings*)

Mwenendo kabidhi unaofanywa kwa mashauri yanayosikilizwa Mahakama Kuu umelalamikiwa kuwa unachelewesha mashauri kwa kuwa mashauri hayo hutumia muda mrefu kutajwa katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya zisizokuwa na mamlaka ya usikilizwaji wa mashauri hayo. Wadau walipendekeza kuondoa utaratibu wa mwenendo kabidhi na badala yake mashauri yafunguliwe moja kwa moja Mahakama Kuu au uwekwe ukomo wa muda wa upelelezi wakati shauri likiwa mahakama isiyokuwa na mamlaka likisubiri upelelezi. Pia, washtakiwa wanaosubiri mashauri yao kusikilizwa Mahakama Kuu walilalamika kutopatiwa jalada lenye maelezo ya mashahidi na vielelezo kwa wakati kwa ajili ya kujiandaa na usikilizwaji wa kesi Mahakama Kuu.

Tume imebaini kwamba, kuondoa moja kwa moja mwenendo kabidhi kwa kufungua mashauri moja kwa moja Mahakama Kuu kunaweza kuchelewesha washtakiwa kufikishwa mahakamani kwa wakati hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya mikoa haina Mahakama Kuu. Vilevile, baadhi ya Wilaya zipo mbali na Makao Makuu ya Mkoa zilipo Mahakama Kuu na hivyo itasababisha watuhumiwa kukaa vituo vya polisi muda mrefu wakisubiri kufikishwa Mahakama Kuu.

Tume imebaini kuwa, tatizo kubwa linaloathiri utaratibu wa mwenendo kabidhi ni ucheleweshwaji wa upelelezi hivyo hata kama mashauri haya yatafunguliwa moja kwa moja Mahakama Kuu pasipo kutatua changamoto za upelelezi itakuwa ni kuhamishia matatizo ya ucheleweshaji wa mashauri Mahakama Kuu na hivyo kutotatua tatizo la msingi.

Tume inapendekeza:

- (i) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura 20, irekebishwe ili kubainisha ukomo wa muda wa upelelezi kwa mashauri yanayosubiriwa kusajiliwa Mahakama Kuu kwa ajili ya usikilizwaji;
- (ii) Vyombo vya uchunguzi au upelelezi viwezeshwe katika rasilimali watu, fedha na vitendea kazi ili viweze kukamilisha upelelezi kwa wakati;
- (iii) Mwenendo wa shauri husika uendeshwe na Hakimu aliyepewa mamlaka ya ziada ya kuendelea na usikilizwaji wa awali mara baada ya kukamilika kwa mwenendo kabidhi kama ilivyoelekezwa katika **Nyaraka za Jaji Kiongozi Na. 1, 2 na 5 za mwaka 2019.**
- (iv) Mahakama na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) wahakikishe washtakiwa wanaosubiri mashauri yao kusikilizwa Mahakama Kuu wanapatiwa jalada lenye maelezo ya mashahidi na vielelezo kwa wakati.

2.12 Usikilizwaji wa Awali (*Preliminary Hearing*)

Katika mnyororo wa usikilizwaji wa shauri la Jinai, hatua hii hujumuisha usikilizwaji wa awali wa kesi ambapo upande wa mashtaka husoma muhtasari wa kesi ikiwemo ushahidi uliopo na kuupa upande wa utetezi nafasi ya kukubali au kukataa ushahidi huo.⁷ Lengo la usikilizwaji wa awali ni kumfanya mshtakiwa aelewe ushahidi wa kesi inayomkabili⁸ na kubainisha hoja zinazobishaniwa baina ya upande wa mashtaka na upande wa utetezi. Hoja zinazobishaniwa ndizo zitakazotolewa ushahidi wakati wa usikilizaji wa shauri ili kuharakisha usikilizaji wa mashauri ya jinai. Baadhi ya wadau wamewasilisha maoni kuwa, usikilizwaji wa awali wa mashauri ya jinai

⁷ Kifungu cha 192 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 na kifungu cha 35(1) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200

⁸ *Uganda v. Okumu Reagan and 5 others, revision no. 003 of 2018*

unachelewesha usikilizwaji wa mashauri hayo na kupendekeza hatua hii iondolewe.

Hata hivyo, ili kuhakikisha usikilizwaji wa mashauri, usikilizaji wa awali ni nyenzo muhimu ya kuiwezesha mahakama kusimamia shauri husika (*case management tool*) na kujua ushahidi unaotarajiwa kuletwa mahakamani wakati wa usikilizaji.

Tume inapendekeza:

- (i) Usikilizwaji wa awali wa mashauri ya jinai uendelee kuwepo katika mfumo wa Haki Jinai wa kisasa (*modern Criminal Justice*) ili mshtakiwa aweze kufahamu ushahidi wa kesi inayomkabili badala ya kupata ushahidi huo kwa kushtukizwa wakati wa usikilizwaji wa shauri.
- (ii) Elimu kwa umma itolewe kuhusu lengo la usikilizwaji wa awali na umuhimu wake katika mnyororo wa Haki Jinai; na
- (iii) Mawakili wa Serikali na wa kujitegemea washirikiane ili kufikia malengo ya usikilizwaji wa awali wa mashauri.

2.13 Malipo ya Mafao ya Mkupuo ya Kustaafu

Katika ziara zilizofanyika, Tume imebaini uwepo wa malalamiko makubwa kutoka kwa askari wa Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi hususani wale wa vyeo vya chini kuhusu mafao ya uzeeni (*kikokotoo*). Msingi wa malalamiko hayo ni kuwa, utaratibu mpya wa kukokotoa mafao ya mkupuo ya kustaafu umeathiri kwa kiasi kikubwa kiwango cha malipo hayo kutokana na malipo yao kuhusisha posho nyingi na umri wa kustaafu kuwa mdogo. Hivyo kusababisha askari kulipwa kiasi cha fedha ambacho hakikidhi mahitaji.

Tume inapendekeza:

- (i) Mishahara ya askari wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza iboreshwe kwa posho za msingi zilizopo kisheria kujumuishwa katika mishahara

yao ili kuwawezesha kupata mafao ya mkupuo yanayoridhisha wakati wa kustaafu; na

- (ii) Umri wa kustaafu kwa askari wenye vyeo vya chini katika Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza uongezwe na kuoanishwa na ule wa watumishi wa umma ili muda wa kuchangia kwenye mfuko wa Pensheni uongezeke.

2.14 Utaratibu wa Ajira Katika Jeshi la Polisi na Magereza

Utaratibu wa kuajiri askari wa Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi kwa kigezo cha kupitia Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi kwa kujitolea umelalamikiwa na wadau kuwa unachangia baadhi ya vijana wenye sifa za kujiunga Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza kukosa nafasi. Aidha, kumekuwepo na malalamiko kutoka upande wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza kuwa, sehemu kubwa ya askari wanaokutwa na changamoto za nidhamu katika vyombo hivyo ni askari walioajiriwa kwa sifa za kupata mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi. Aidha, kigezo hiki kinalikosesha Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi kupata watumishi wenye vipaji ambao hawakupitia Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi.

Tume inapendekeza:

- (i) Suala la kupitia Mafunzo ya JKT na JKU kwa kujitolea lisiwe kigezo cha msingi cha kujiunga na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza hasa katika ajira za utaalamu kama vile udaktari na uhandisi, isipokuwa kigezo hicho kinaweza kuwa kigezo cha ziada;
- (ii) Mifumo ya ajira ndani ya Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza ipitiwe upya ili kuendana na wakati; na
- (iii) Uwazi katika ajira za Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza uimarishwe.

2.15 Maadili na Rushwa

Tume imebaini kuwa, yapo malalamiko mengi toka kwa wananchi dhidi ya taasisi za Haki Jinai ikiwemo ukosefu wa huduma bora kwa mteja, utoaji wa lugha chafu, kuvujisha siri za wateja, matumizi ya nguvu na vitisho kwa watuhumiwa, watuhumiwa kunyimwa haki za msingi, kushindwa kuchukua hatua stahiki uhalifu unapotokea, upendeleo katika kuajiri na ulevi na ukinzano wa maslahi baina ya watendaji na wafadhili (wadau werevu).

Aidha, Tume ilipokea malalamiko kutoka kwa askari na wananchi kuhusu vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi wa watumishi wa Taasisi za Haki Jinai ili waweze kutoa huduma mbalimbali. Mathalani Tume ilibaini kuwepo kwa vitendo vya rushwa katika ajira, upandishwaji wa vyeo, upelelezi wa mashauri ya jinai ili kuharibu ushahidi na rushwa kwa ajili ya kutoa maamuzi kwa upendeleo.

Tume inapendekeza:

- (i) Taasisi za Haki Jinai ziboreshe mifumo ya ndani katika kubaini na kuwawajibisha watumishi wake kwa vitendo vya utovu wa nidhamu;
- (ii) Taasisi za Haki Jinai ziwezeshe kutoa mafunzo ya maadili ya mara kwa mara kwa watumishi wake;
- (iii) Kamati za maadili ziimarishwe na kutambulika kisheria ili zimsaidie mwajiri kuchukua hatua stahiki kwa wafanyakazi watakaobainika kuhusika na vitendo vya uvunjifu wa maadili ikiwemo kutoa na kupokea rushwa;
- (iv) Mifumo ya TEHAMA iimarishwe ili kuboresha utendaji; na
- (v) Taasisi zitengewe bajeti toshelevu ili kuziepusha na utegemezi kwa wadau werevu.

2.16 Wenye Mahitaji Maalumu Katika Mfumo Wa Haki Jinai

Tume ilitembelea Taasisi za Haki Jinai ikiwemo Mahakama, Vituo vya Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Magereza na kubaini upungufu wa wataalam wa lugha za alama na nukta nundu, na miundombinu na vitendea kazi rafiki kwa wenye mahitaji maalumu.

Kutokana na mapungufu yaliyobainika, imeonekana wazi kundi la wenye mahitaji maalumu linapitia changamoto katika mnyororo wa Haki Jinai kwa kukosa huduma bora kadri ya mahitaji yao hasa ikizingatiwa kuwa ni miongoni mwa waathirika wa vitendo vya jinai hususan ukatili wa kijinsia.

Tume inapendekeza:

- (i) Taasisi za Haki Jinai ziajiri wataalamu wa lugha za alama na maandishi ya nukta nundu, wataalamu wa afya ya akili na ustawi wa jamii ili kuimarisha huduma kwa wenye mahitaji maalumu;
- (ii) Taasisi za Haki Jinai ziweke miundombinu rafiki, vitendea kazi, vifaa saidizi na mahitaji mengine muhimu ili kuwezesha wenye ulemavu kupata huduma stahiki katika mnyororo wa Haki Jinai.

2.17 Mfuko wa Kufidia Waathirika wa Uhalifu

Tume ilipokea maoni ya wadau kuwa, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai katika kifungu cha 37 inatoa haki ya fidia kwa mwathirika anayemsaidia hakimu, askari au afisa mwingine wa sheria kuzuia kosa lisitendeke au ukamataji wa mhalifu na endapo atafariki wategemezi wake watafidiwa. Ilielezwa zaidi kuwa, CPA katika vifungu vya 348 na 348A vinaipa Mahakama mamlaka ya kumtaka mshtakiwa kulipa fidia kwa mwathirika wa uhalifu alioufanya. Utaratibu wa fidia uliowekwa kwa mujibu wa vifungu hivi ni mgumu kutekelezeka kwa kuwa washitakiwa wengine hawana uwezo wa kulipa fidia kwa waathirika. Hivyo, wadau walipendekeza kuanzishwa kwa mfuko maalumu wa fidia utakaotumika kuwafidia waathirika wa jinai.

Tume ilifanya uchambuzi wa maoni yaliyopokelewa kwa kuzingatia uzoefu wa nchi nyingine na taarifa za tume nyingine ambapo ilibainika kuwa, katika nchi za Uingereza, India na Kenya, kuna mifuko maalum kwa ajili ya kufidia waathirika wa uhalifu. Aidha, Ripoti ya Tume ya Msekwa ya mwaka 1977 ilibaini umuhimu wa kuanzisha mfumo wa kisheria wa kuhudumia waathirika wa makosa ya jinai. Kufuatia maoni ya Tume hiyo, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, mwaka 1987 ilishauri mfuko wa fidia kwa waathirika uanzishwe.

Tume inapendekeza:

Maoni yaliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania ya mwaka 1987, kuhusu kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Waathirika wa Uhalifu yatekelezwe.

2.18 Adhabu ya Kifungo cha Maisha

Tume imepokea malalamiko kutoka kwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha maisha wakilalamika kuwa kifungo cha maisha hakiwapi nafasi ya pili ya kurekebika na kuendelea kulitumikia Taifa. Hivyo, walipendekeza kuwa kifungo cha maisha kiwe na ukomo ili kuwawezesha kujua hatma yao wakiwa gerezani.

Tume imetathmini sheria zinazohusiana na hukumu ya kifungo cha maisha kinachotekelezwa kwa mfungwa kubaki gerezani kwa maisha yake yote ya asili au kwa muda usiojulikana hadi asamehewe, aachiliwe, au abadilishiwe kifungo. Adhabu ya kifungo cha maisha ni ya lazima kwa makosa ya ulawiti, ubakaji unaofanywa na kikundi cha watu, ubakaji wa mtoto mwenye umri chini ya miaka 10, usafirishaji wa dawa za kulevya na kufadhili usafirishaji wa dawa za kulevya.

Uzoefu kutoka nchi nyingine unaonesha kuwa, baadhi ya nchi kama Brazil imefuta adhabu ya kifungo cha maisha na adhabu ya mwisho ni kifungo cha miaka 40, mamlaka nyingine kama Afrika Kusini na baadhi ya majimbo nchini

Marekani na Australia zimeainisha muda ambao mfungwa atatumikia kifungo cha maisha gerezani ili aweze kustahiki adhabu mbadala ya kuwa chini ya uangalizi (*Parole*). Aidha, nchini Mauritius adhabu ya kifungo cha maisha (*Servitude for life*) imetafsiriwa ni kifungo kisichozidi miaka 60.

Tume inapendekeza:

Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura 16, irekebishwe ili kuweka tafsiri ya kifungo cha maisha.

2.19 Adhabu ya Kifo

Maoni mbalimbali yamewasilishwa kwa Tume kuhusu utekelezaji wa adhabu ya kifo nchini. Baadhi ya wadau walipendekeza adhabu ya kifo isiondolewe katika sheria kwa sababu ni adhabu stahiki kwa makosa yaliyotendwa na mhusika na adhabu hiyo ni funzo kwa jamii kutokutenda makosa ambayo adhabu yake ni kifo. Wadau wengine walipendekeza adhabu ya kifo iondolewe kwa kuwa, ni ya kikatili na isiyozingatia haki ya kuishi. Vilevile, Tume imebaini kuwa, adhabu hiyo imekuwa haitekelezwi kwa miaka mingi hivyo kusababisha waliopewa adhabu hiyo kuishi maisha ya hofu huku wakisubiri utekelezaji wa adhabu hiyo. Kwa takwimu za mwezi Mei, 2023, wanaosubiria kunyongwa ni 691.

Tume ilifanya uchambuzi wa maoni yaliyowasilishwa na pia kuangalia uzoefu wa nchi nyingine kama India na Marekani. Uzoefu huu umebainisha kuwa katika baadhi ya nchi makosa ya mauaji yanasikilizwa na kuhitimishwa na mahakama ikiwemo kutoa hati ya utekelezaji wa adhabu ya kifo. Hata hivyo, Rais wa nchi husika anaweza kutoa msamaha au kumbadilishia adhabu mtu aliyehukumiwa adhabu ya kifo kwa mujibu wa katiba ya nchi husika.

Tume inapendekeza:

- (i) Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, ifanyiwe marekebisho ili adhabu ya kifo isiwe adhabu pekee kwa kosa la mauaji bali adhabu itolewe kulingana na mazingira ya utendaji kosa⁹; na
- (ii) Adhabu ya kifo isiporidhiwa na Mheshimiwa Rais kwa kipindi cha miaka mitatu, adhabu hiyo itenguke kuwa kifungo cha maisha.

2.20 Matumizi ya TEHAMA Katika Upelelezi na Uendeshaji wa Mashtaka

Matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za haki jinai yanakabiliwa na changamoto ya mifumo ya TEHAMA kutosomana baina ya Taasisi za Haki Jinai, ukosefu wa miundombinu na ukosefu wa wataalam, upungufu wa vitendea kazi vya kisasa katika uzuiaji, kubaini na kupeleleza makosa ya jinai. Hali hiyo inasababisha ucheleweshaji wa upelelezi, upelelezi usiokidhi viwango na ucheleweshaji wa usikilizwaji wa mashauri.

Tume inapendekeza:

- (i) Uwepo Mfumo Jumuishi wa Haki Jinai unaosomana utakaounganisha Taasisi za Haki Jinai utakaosaidia katika kubadilishana taarifa;
- (ii) Taasisi za Haki Jinai ziwezeshe kufanya uwekezaji kwenye eneo la miundombinu ya TEHAMA na usimikaji wa mifumo ya kidijitali;
- (iii) Taasisi za Haki Jinai ziwezeshe kuajiri wataalamu wa TEHAMA na kuwaendeleza kwa mafunzo ili waweze kusimamia na kutoa msaada wa kiufundi; na
- (iv) Watumishi wa Taasisi za Haki Jinai wawezeshe kupatiwa vifaa vya kisasa vya TEHAMA ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

⁹ Ali Rajabu & Others v. United Republic of Tanzania ACHPR Case. No. 007/2015

3.0 MAPENDEKEZO MAHUSUSI KWA TAASISI

3.1 Jeshi la Polisi

3.1.1 Taswira ya Jeshi la Polisi

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi kuhusu vitendo vinavyochafua taswira ya Jeshi la Polisi. Malalamiko hayo dhidi ya Jeshi la Polisi yanahusu kushindwa kuzuia uhalifu, matumizi ya nguvu kupita kiasi, kubambikia kesi, vitendo vya rushwa, mali za watuhumiwa kupotea vituoni na kuchelewa kufika kwenye maeneo ya matukio. Hali hiyo inasababisha wananchi kupoteza imani kwa Jeshi la Polisi na kutokutoa ushirikiano unaotakiwa.

Tume inapendekeza:

- (i) Jeshi la Polisi lifanyiwe tathmini ya kina itakayoweza Jeshi hilo kufanyiwa maboresho makubwa na kuundwa upya ili kuondoa kasoro za kiutendaji zilizopo;
- (ii) Jeshi la Polisi libadilishwe kisheria, kimuundo na kifikra na kuwa Polisi Tanzania (*National Police Service*) ili kutoa taswira kuwa Jeshi la Polisi ni chombo cha kuwahudumia wananchi;
- (iii) Kubadilisha mitaala ya mafunzo na mtazamo wa askari wa Jeshi la Polisi ili kutoka katika dhana ya ujeshi (*police force*) kwenda dhana ya kuhudumia wananchi (*police service*);
- (iv) Jeshi la Polisi liboreshe mfumo wa ndani wa kushughulikia malalamiko ya wananchi; na
- (v) Jeshi la Polisi liimarisha huduma za Intelijensia ya jinai na Polisi Jamii na kuanzisha programu za kuisogeza zaidi kwenye jamii.

3.1.2 Matumizi ya Amri Kuu za Jeshi la Polisi (PGO)

Katika kufanya tathmini juu ya Jeshi la Polisi, Tume ilipitia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayoliongoza Jeshi la Polisi. Tume ilibaini kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi kupitia kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi¹⁰ amepewa mamlaka ya kutunga Amri Kuu za Jeshi la Polisi kwa kuzingatia maelekezo na amri za Waziri mwenye dhamana ya mambo ya ndani ya nchi. Uchambuzi wa Tume umebaini kuwa PGO iliyotangazwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 351 la Mwaka 2021 imetengenezwa pasipo kuzingatia masharti na wigo wa kisheria uliopo katika kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi na Sheria nyingine. Baadhi ya maeneo yaliyoonekana kuwa na changamoto kubwa ni masuala ya posho za askari, mamlaka za nidhamu, uchunguzi wa vifo vyenye utata, gwaride la utambuzi wa mhalifu, mafao ya kustaafu kwa Makamishna wa Jeshi la Polisi na ukokotoaji wa mafao ya kustaafu kwa Askari, Wakaguzi na Maafisa.

Tume inapendekeza:

- (i) Kwa kuwa imebainika PGO GN. Na. 351/2021 inayotumika sasa iliandaliwa pasipo kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu; Serikali isitishie matumizi yake na PGO iliyokuwepo awali iendelee kutumika; na
- (ii) Kwa kuzingatia changamoto zilizomo ndani ya PGO, yafanyike pia mapitio ya Kanuni za Kudumu za Jeshi la Magereza (PSO) za Mwaka 2003, Amri Kuu za Idara ya Uhamiaji (IGO) za Mwaka 2023 na Kanuni Kuu za Jeshi Usu la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misititu.

¹⁰ Sura ya 322

3.1.3 Usimamizi wa Usalama Barabarani

Yapo malalamiko kutoka kwa wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu changamoto zitokanazo na matumizi ya barabara na vyombo vya usafiri. Miongoni mwa malalamiko hayo ni udhibiti wa usalama barabarani kufanywa na taasisi zaidi ya moja kama vile TARURA, TANROADS, LATRA Halmashauri na Jeshi la Polisi. Miongoni mwa Taasisi hizo zipo zinazotoa adhabu tofauti kwa kosa moja, mathalani LATRA na Jeshi la Polisi katika kosa la mwendokasi.

Vilevile, kuna malalamiko kuhusu kuwepo kwa waendesha pikipiki za abiria (*Bodaboda*) wasiokuwa na mafunzo wala leseni za udereva, vitendo vya rushwa na mchakato mrefu wa fidia kwa wanaopata ajali. Aidha, kuna ongezeko la ajali za barabarani kutokana na ubovu wa vyombo vya moto vya usafiri na miundombinu.

Tume inapendekeza:

- (i) Kuwianisha (*harmonize*) sheria za usimamizi wa usalama barabarani. Mathalani, adhabu ya kosa la kuzidisha mwendo chini ya Sheria ya LATRA ni tofauti na ile inayotolewa na Sheria ya Usimamizi wa Usalama Barabarani, Sura ya 168, kwenye suala la adhabu;
- (ii) Leseni za udereva zisihuishwe kwa madereva wanaoonekana kuwa wakosaji sugu wa makosa ya usalama barabarani;
- (iii) Mifumo ya makosa ya usalama barabarani ya Jeshi la Polisi na Mifumo ya Utoaji wa leseni za udereva ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) isomane ili kuwabaini madereva wakosaji sugu;
- (iv) Taasisi zitakazohitaji kufanya shughuli zinazohusiana na usalama barabarani zishirikiane na Askari wa Usalama barabarani;
- (v) Uwekwe utaratibu endelevu unaolazimisha ukaguzi wa vyombo vya moto kulingana na aina na matumizi;

- (vi) Ufanyike utafiti kuona uwezekano wa kuweka utaratibu wa malipo ya fidia kwa waathirika wa ajali ili Kampuni za Bima zimlipe muathirika kwanza kisha taratibu nyingine ziendeleo baina ya Kampuni ya Bima na mmiliki wa chombo cha usafiri;
- (vii) Lianzishwe dawati maalum kwenye Jeshi la Polisi kushughulikia waathirika wa ajali, wakadiria hasara na kampuni za bima wanapohitaji ufafanuzi au marekebisho ya nyaraka zinazotolewa na Polisi;
- (viii) Malipo ya huduma za bima ya magari (*premium*) yafanyike kulingana na historia ya ajali ya mkata bima badala ya kuwa kiwango sawa kwa watu wote bila kuzingatia historia yao ya kusababisha ajali;
- (ix) Udhibiti wa usalama barabarani ufanyike kwa kutumia vifaa vinavyojiendesha (*automation*). Shughuli hii ifanyike kwa ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi (PPP); na
- (x) Iandaliwe kanzidata (*database*) ya bajaji na bodaboda ili iwe rahisi kuwatambua, kuwaratibu na kuwasimamia wamiliki, madereva na vyombo vyao, mathalani kwa kutoa rangi na namba ya utambuzi. Aidha, kanzidata hiyo itasaidia pia katika utoaji wa mafunzo na leseni kwa madereva wa bodaboda na bajaji .

3.1.4 Uwajibikaji na Usimamizi Huru wa Jeshi la Polisi

Tume ilipokea malalamiko ya kuwepo kwa matukio mengi ya ukiukwaji wa Sheria unaofanywa na watendaji wa Taasisi za Haki Jinai hususan Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na matumizi ya nguvu kupita kiasi wakati wa ukamataji, kutesa watuhumiwa wakati wa kuchukua maelezo ya onyo, na kubambikia watu kesi.

Tume inapendekeza:

- (i) Madawati ya Malalamiko ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi yaimarishwe kwa kuyapatia watumishi wa kutosha wenye weledi kwenye masuala ya uchunguzi ili waweze kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa kwenye Taasisi hizo ipasavyo; na
- (ii) Ili kushughulikia nidhamu na maadili ya askari na maafisa, muundo wa Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji uangaliwe ili kiwe chombo kinachotekeleza majukumu yake kila siku badala ya kutekeleza majukumu yake kwa vikao.

3.2 Jeshi la Magereza

3.2.1 Taswira ya Jeshi la Magereza

Tume imepokea maoni kutoka kwa wadau na wananchi kuhusu matumizi ya nguvu, ukaguzi unaotweza utu, uwepo wa msongamano wa wafungwa, mahabusu na wazuiliwa, uchakavu wa miundombinu na kukosekana kwa mabadiliko chanya ya wahalifu wanaomaliza kutumikia vifungo vyao kama ilivyotarajiwa. Hali hiyo inasababisha Jeshi la Magereza kulalamikiwa kwa ukiukwaji wa haki za Binadamu.

Tume inapendekeza:

- (i) Jina la Jeshi la Magereza lifanyiwe marekebisho ya kisheria, kifikra na kimiundo kutoka kuwa sehemu ya kutoa huduma ya kuhifadhi wafungwa (*Prison Services*) na kutoa huduma ya urekebishaji (*correctional services*);
- (ii) Mitaala ya mafunzo ya askari magereza irekebishwe ili iendane na mabadiliko ya kutimiza majukumu ya urekebishaji ipasavyo;

- (iii) Kuwapo Magereza mahususi kulingana na shughuli za kiuchumi kama viwanda, kilimo, ufugaji na biashara ili kuwawezesha wafungwa kujifunza na kuendeleza vipawa walivyonavyo;
- (iv) Utaratibu wa ajira uwezeshe kupatikana kwa watendaji wenye ujuzi na maarifa wa kutimiza majukumu kuendana na uanzishwaji wa taasisi ya Huduma za Urekebishaji.
- (v) Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, liandae mfumo ikiwemo ya TEHAMA wa kufuatilia wafungwa waliotoka gerezani ili kuhakikisha wanatangamana na jamii baada ya kumaliza kifungo;
- (vi) Kuwe na mfumo wa kutafuta masoko ya bidhaa zinazotengenezwa na wafungwa magerezani; na
- (vii) Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Chuo cha Ustawi wa Jamii waandae mafunzo kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada kwa askari Magereza kuhusiana na urekebishaji wa wafungwa.

3.3 Huduma za Wafungwa na Mahabusu Gerezani

Kumekuwa na malalamiko kuhusu ufanisi wa huduma wanazopewa wafungwa na mahabusu wakiwa magerezani, mathalani huduma za afya, ubora wa chakula, huduma za kiroho, kisheria na ukaguzi usio na staha. Vilevile, uwezo mdogo wa magereza ikilinganishwa na idadi ya wafungwa na mahabusu (msongamano), watoto waliokinzana na sheria kuwekwa kwenye mahabusu za watu wazima, uchakavu wa miundombinu ya magereza, kutokuwepo kwa miundombinu rafiki kwa wenye mahitaji maalum, kutokuwepo kwa magereza katika baadhi ya wilaya ambazo kuna Mahakama na vituo vya Polisi na kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika wa kuwapeleka mahabusu na wafungwa mahakamani. Pia, matumizi makubwa ya nishati inayotokana na kuni yanayosababisha uharibifu wa mazingira na wafungwa kutumia muda mwingi kutafuta kuni ni miongoni mwa mambo

yanayolalamikiwa. Malalamiko hayo yamesababisha kuonekana kwamba huduma za Magereza hazijali utu wa wafungwa na mahabusu pamoja na kuchelewesha upatikanaji wa haki zao.

Tume inapendekeza:

- (i) Tathmini ya kina ifanyike na ripoti iandaliwe, wakati mfungwa akianza kutumikia kifungo chake gerezani ili kubaini mahitaji yake ya kisaikolojia, kiafya, kielimu na kidini na matarajio yake ya kujiendeleza kimaisha na uwezekano wa mfungwa kutangamana na jamii na kupangiwa Gereza atakaloweza kutimiza ndoto zake na kuendeleza vipaji na kazi yake (uzoefu uchukuliwe kutoka kifungu 38 cha sheria ya *Correctional Services Act No. 111 of 1998* ya Afrika Kusini);
- (ii) Katika kipindi kisichozidi miaka miwili magereza yote yawezeshwe kutumia nishati nyingine kama umeme, gesi asilia na masalia ya mimea na vinyesi vya wanyama (*Biogas* na *Biomass*) katika kupikia ili kulinda afya na kuhifadhi mazingira;
- (iii) Kuwepo na maafisa magereza ambao ni wataalamu wa ustawi wa jamii ili waweze kutoa huduma za kisaikolojia kwa wafungwa kama njia ya urekebu;
- (iv) Utolewaji wa huduma ya msaada wa kisheria, kiroho na kisaikolojia kwa wafungwa na mahabusu uimarishwe na sheria ya huduma ya msaada wa kisheria irekebishwe kuendana na hilo;
- (v) Ili kufuatilia mienendo magerezani, Jeshi la Magereza liwezeshwe kufunga mitambo ya kisasa ya ukaguzi wa wafungwa na mahabusu ili kufanya ukaguzi wenye kuzingatia utu na staha ya binadamu;
- (vi) Kuwepo kwa vyumba mahususi kwa ajili ya kufanyia upekuzi wa wafungwa na mahabusu utaozingatia faragha na staha;

- (vii) Jeshi la Magereza liwezeshe kukarabati magereza kwa kuwa magereza mengi yamechakaa ikizingatiwa kuwa yalijengwa wakati wa ukoloni;
- (viii) Elimu kwa umma itolewe kuhusu matumizi ya adhabu mbadala kwa wadau wote ili iweze kutumika na kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani;
- (ix) Jeshi la Magereza lishirikiane na Wizara ya Elimu na Ufundi, Chuo Kikuu Huria (OUT), *Vocational Education and Training Authority* (VETA) na *Folk Development College* (FDC) kuandaa mitaala na kutoa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma na mafunzo ya ufundi stadi kwa wafungwa kadri ya uwezo wao. Aidha, utaratibu huu uendane na kuainisha magereza yote nchini kulingana na stadi za ufundi na uzalishaji zinazoweza kupatikana katika magereza hayo;
- (x) Kwa kuwa msongamano wa wafungwa upo kwenye baadhi ya magereza, Jeshi la Magereza litumie taratibu ilizonazo kuhamisha wafungwa kutoka magereza yenye msongamano kwenda kwenye magereza yasiyokuwa na msongamano;
- (xi) Jeshi la Magereza liandae mkakati mahsusi wa urekebishaji wa wafungwa;
- (xii) Jeshi la Magereza liwezeshe kutekeleza jukumu lake la kuwapeleka mahabusu na wafungwa mahakamani;
- (xiii) Ufanyike utafiti wa kuangalia uwezekano wa wafungwa kukatiwa bima za afya za makundi (*Group Health Insurance Fund*) kwa mfano CHF;
- (xiv) Kwa kushirikiana na *International Organisation for Migration* (IOM) Serikali ifanye utaratibu wa kuwarudisha kwenye nchi zao Wazuiliwa

(hususun kutoka nchi ya Ethiopia) waliomaliza vifungo vyao waliopo magerezani;

- (xv) Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na halmashauri ambazo hazina magereza zijenge magereza katika Wilaya hizo;
- (xvi) Kuongeza matumizi ya adhabu mbadala; na
- (xvii) Zijengwe kumbi za kusikiliza kesi kwa njia ya mitandao.

3.4 Huduma ya Ustawi wa Jamii

Katika mfumo wa Haki Jinai, maafisa ustawi wa jamii wana jukumu muhimu la kusimamia mahabusu za watoto na shule za maadilisho, kushiriki katika mahakama za watoto na mahakama za kawaida, kwenye utoaji wa amri za huduma kwa jamii na kuandaa ripoti za uchunguzi wa kijamii. Pamoja na umuhimu wa jukumu hilo, Tume imebaini kuwa Idara ya Huduma za Ustawi wa Jamii inakabiliwa na upungufu wa rasilimali watu na rasilimali fedha, uchache wa nyumba salama katika baadhi ya maeneo na muundo usiokidhi mahitaji ya utekelezaji wa majukumu ya Haki Jinai.

Tume inapendekeza:

- (i) Idara ya Ustawi wa Jamii ipandishwe hadhi na kuwa idara inayojitegemea ndani ya Wizara yenye dhamana na ustawi wa jamii ili iweze kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa urahisi kwenye Taasisi za Haki Jinai na wananchi kwa ujumla;
- (ii) Huduma za Ustawi wa Jamii ziwezeshe katika rasilimali watu na fedha na ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
- (iii) Mahabusu za watoto na shule za maadilisho ziongezwe ili kuepusha watoto waliokinzana na sheria kuchanganyika na watu wazima; na
- (iv) Kila Mkoa uweke mkakati wa kujenga shule moja ya maadilisho kwa kuzishirikisha Halmashauri zilizopo katika Mkoa husika.

3.5 Idara ya Uangalizi

Divisheni ya uangalizi ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. majukumu ya Divisheni hiyo ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa adhabu mbadala Tanzania Bara kupitia Sheria ya Uangalizi wa Wafungwa, Sura ya 247, (*The Probation of Offenders Act, Cap. 247*) na Sheria ya Huduma kwa Jamii Sura 291 (*The Community Service Act, Cap. 291*).

Tume imebaini kuwa, bado hakuna matumizi ya kuridhisha adhabu mbadala jambo ambalo linasababisha msongamano wa wafungwa magerezani na hivyo kuongeza gharama za kuwahudumia wafungwa husika. Aidha, kumekuwapo na mtazamo hasi kwa wananchi kuhusu adhabu mbadala na hivyo kutoona umuhimu wake.

Tume inapendekeza:

- (i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iwezeshe kwa rasilimaliwatu na fedha ili kuimarisha Idara ya Uangalizi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
- (ii) Mahakama, Jeshi la Magereza na Taasisi nyingine za Jinai ziongeze matumizi ya adhabu mbadala pale panapostahili; na
- (iii) Elimu itolewe kwa wadau wote muhimu na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa adhabu mbadala ili kubadili mtazamo kuwa adhabu ni kifungo cha gerezani pekee.

3.6 Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina nafasi kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya haki jinai katika kufanikisha upelelezi hasa mashauri yanayohitaji uchunguzi wa sampuli.

Tume imepokea malalamiko kutoka Taasisi za Upelelezi na Uchunguzi kuwa Mamlaka hiyo inatoza gharama kubwa za uchunguzi wa sampuli, inachelewesha taarifa za matokeo ya uchunguzi na haipo kwenye ngazi za

mkoa na wilaya, hali inayoathiri uwezo wa Mamlaka hiyo kuhudumia Taasisi za Haki Jinai.

Kwa upande mwingine, Mamlaka imezilalamikia Taasisi za Upelelezi na Uchunguzi kuwa hazifuatili matokeo ya uchunguzi wa sampuli zinazowasilishwa kwenye Mamlaka hiyo na haziwalipi posho kwa wakati watumishi wa Mamlaka hiyo wanapoenda kutoa ushahidi mahakamani .

Tume inapendekeza:

- (i) Uanzishwe mfumo jumuishi wa TEHAMA utakaosaidia kufuatilia mwenendo wa vielelezo kutoka taasisi moja kwenda nyingine;
- (ii) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iwezeshwe ili iweze kuwalipa mashahidi wanaotoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na mashahidi wengine kwa wakati;
- (iii) Matumizi ya *video conferencing* katika kutoa ushahidi yahamasishwe hususani kwa watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuwawezesha watumishi hao kutekeleza majukumu mengine;
- (iv) Gharama za uchunguzi wa sampuli kutoka Taasisi za Haki Jinai zilipwe na Serikali moja kwa moja kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;
- (v) OTU itakapoanzishwa, ijengewe maabara ya kisasa inayojitosheleza na yenye wataalamu wa kutosha; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ibaki na jukumu la kuwa msimamizi na mamlaka ya rufaa.

3.7 Mahakama ya Tanzania

Kumekuwepo na malalamiko kuhusu ucheleweshaji wa kusikiliza mashauri katika Mahakama Kuu. Tume ilibaini kuwa kuna mashauri mengi zaidi ya 1000 ambayo yamefungwa na yanasubiri kusikilizwa na Mahakama Kuu.

Tume inapendekeza:

- (i) Mahakama na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka waandae mkakati wa pamoja wa kusikiliza mashauri ambayo upelelezi wake umekamilika;
- (ii) Mahakama na Ofisi ya Mashtaka ya Taifa ziwezeshe ili kuharakisha usikilizwaji wa mashauri; na
- (iii) Wizara ya Katiba na Sheria na Mahakama ihakikishe Kamati za Kusukuma Kesi na Jukwaa la Haki Jinai yanatumika ipasavyo na kwa ufanisi.

3.8 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB)

Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 6 (1) (a) hadi (o) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391, inataja majukumu ya Tume. Pamoja na majukumu mengine, Tume ina jukumu la kufanya uchunguzi kuhusu masuala yanayohusu uvunjaji wa Haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Mbali na kuwapo kwa Tume, kumekuwapo na mapendekezo kutoka kwa wadau ya kuanzisha chombo kipya na huru cha kiraia kwa ajili ya kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya taasisi zinazohusika na Haki Jinai.

Tume imebaini kuwa pamoja na kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ripoti za Tume hiyo hazitekelezwi na taasisi zinazo lalamikiwa.

Tume inapendekeza:

- (i) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ianzishe divisheni maalumu itayoshughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu taasisi za Haki Jinai na watendaji wake;

- (ii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iwezeshe kwa rasilimali watu na fedha ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
- (iii) Mifumo ya utekelezaji wa ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ifanyiwe tathmini ili kuangalia namna bora ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti;
- (iv) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itumie mamlaka yake ya kisheria chini ya Kifungu cha 6(1)(e) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391, kuchukua hatua za kisheria na kushughulikia ukiukaji wa haki za binadamu inazozichunguza;
- (v) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itoe elimu kwa umma ili wananchi waweze kujua majukumu ya Tume na hivyo kutoa ushirikiano; na
- (vi) Ripoti za divisheni maalumu ya Tume itayoshughulikia malalamiko ya wananchi ziwasilishwe kwa Rais kupitia Katibu Mkuu Kiongozi ambaye ni Mkuu wa Utumishi wa Umma.

3.9 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Lengo la Serikali katika kutenganisha mashtaka na upelelezi linakabiliwa na changamoto ya kutokuwepo kwa Ofisi za mashtaka katika wilaya 96 nchini. Aidha, kuna changamoto ya mashtaka kuendelea kuendesha na waendesha mashtaka kutoka taasisi nyingine ambazo zinajihusisha na upelelezi. Changamoto nyingine ni kutokuwa na uwiano wa idadi kati ya mawakili wa Serikali wanaoendesha mashtaka na mahakimu, majaji na wasajili; ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi, kutokuwepo kwa mfumo wa motisha na maslahi duni ya watumishi. Hali hii inasababishwa na ufinyu wa bajeti na upungufu wa rasilimali watu.

Tume inapendekeza:

- (i) Halmashauri za Wilaya nchini zitoe ofisi za muda kwa ajili ya shughuli za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Wilaya husika;
- (ii) Polisi wanaoendesha mashtaka ambao wana sifa za kuwa mawakili wa Serikali wahamishiwe Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;
- (iii) Serikali iwezeshe Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kufungua ofisi katika wilaya zilizobakia; na
- (iv) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iwezeshe kwa rasilimali ili iweze kukamilisha programu ya utenganishaji wa mashtaka na upelelezi na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba na Sheria.

3.10 Changamoto za Ujumla za Taasisi za Haki Jinai

Katika kutembelea na kuwasikiliza wadau wa Haki Jinai, Tume imebaini kuwa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka zinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti, ukosefu wa vitendea kazi, upungufu wa rasilimali watu, ukosefu wa mafunzo, kutoenea kwa baadhi ya Taasisi katika mikoa na wilaya nchini, maslahi yasiyojitosheleza kwa watumishi na kukosa majengo ya ofisi. Changamoto nyingine ni miundombinu iliyochakaa, kukosa nyumba za makazi kwa watumishi na malalamiko ya matumizi mabaya ya madaraka. Tume imebaini uwepo wa malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi kuhusu taasisi hizo kutoa huduma zisizoridhisha, ukosefu wa maadili na vitendo vya rushwa.

Tume pia imebaini kuwepo kwa tatizo la kibajeti kwenye eneo la upelelezi. Mathalan, fedha zinazotolewa kwa Wilaya na Mkoa kwa mwezi kwa ajili ya upelelezi ni Shilingi 150,000.00 na Shilingi 500,000.00 sawa na Shilingi 5,000.00 na Shilingi 16,600.00 kwa siku mtawalia. Aidha, mafuta yanayotolewa kwa ajili ya shughuli za upelelezi ni lita 10 kwa siku kwa Wilaya zote nchini. Kiasi

hiki cha mafuta kinatolewa bila kuzingatia umbali, ukubwa idadi ya watu na hali ya uhalifu katika Wilaya. Vilevile, ilibainika kuwa, askari polisi na askari magereza wanadai malimbikizo ya stahili na posho mbalimbali ikiwemo za uhamisho, likizo, posho ya kujikimu na nauli.

Kwa heshima na taadhima, Tume inaikumbusha Serikali kuwa Mfumo wa utendaji wa Taasisi za Haki Jinai ni jukumu la msingi la Serikali yoyote inayoamini katika utawala bora na haki za raia. Hivyo, Serikali iweke uzito unaostahili kwa Taasisi za Haki Jinai ili ziongezewe watu wenye utaalamu, weledi na uadilifu wa hali ya juu, kisha wawezeshwe kwa mafunzo, vitendea kazi na mazingira wezeshi ya kutekeleza jukumu hilo.

Tume inapendekeza:

- (i) Wizara ya Fedha na Mipango ishirikiane na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza kutathmini mahitaji ya taasisi hizo na kuona uwezekano wa kuziwezesha kibajeti kulingana na hali halisi;
- (ii) Serikali ilipe madeni yaliyohakikiwa ya Askari, Wakaguzi na Maafisa wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza; na
- (iii) Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wa Taasisi za Haki Jinai.

4.0 MASUALA MAHSUSI YA TANZANIA - ZANZIBAR

Tume ilifanya ziara Tanzania – Zanzibar kwa lengo la kujifunza jinsi ya mifumo ya Haki Jinai inavyoendeshwa. Katika ziara hiyo, Tume ilifanya mazungumzo na Viongozi Wakuu na baadhi ya Viongozi Wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilitembelea Taasisi mbalimbali zinazohusika na Mifumo ya Haki Jinai na ilifanya mikutano na wananchi pamoja na watumishi wa vyombo vya Haki Jinai. Kupitia ziara hiyo, Tume ilipokea changamoto, maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu hali halisi ya mfumo na Taasisi za Haki Jinai Tanzania – Zanzibar kama ifuatavyo:-

4.1 Msamaha wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wanafunzi waliofungwa Tanzania Zanzibar

Tume ilipokea maoni ya wadau kuhusu wanafunzi waliopo katika Vyuho vya Mafunzo - Tanzania Zanzibar kutonufaika inapotokea Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania anaposamehe wafungwa licha ya kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Wadau walipendekeza, Mheshimiwa Rais atumie mamlaka yake hasa kwa wanafunzi ambao hukumu zao zimejadiliwa na kuthibitishwa na Mahakama ya Rufani kupata haki ya msamaha wa Rais kama ilivyo kwa wafungwa walioko Tanzania Bara.

Tume ilifanya uchambuzi wa hoja iliyowasilishwa kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 59 na 60 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Toleo la 2010, Sheria ya Masuala ya Ofisi ya Rais, Sura ya 9. Ibara ya 45 ya Katiba ya Jamhuri Muungano inampa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa msamaha kwa wafungwa. Ibara 45 (3) inabainisha masharti ya matumizi ya mamlaka hayo kwa upande wa Tanzania Zanzibar kuwa, mwenye haki ya msamaha wa Rais ni mwanafunzi aliyehukumiwa na kuadhibiwa Tanzania Zanzibar kwa Sheria inayotumika pande zote za Muungano. Hivyo, kwa msingi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais anaweza tu kutoa msamaha kwa upande wa Tanzania Zanzibar ikiwa sheria iliyotumika inagusa pande zote za muungano na si aina ya mahakama iliyotoa hukumu.

Ibara ya 59 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, imeweka utaratibu wa Rais wa Zanzibar kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyehukumiwa kwa kosa lolote ndani ya Tanzania Zanzibar.

Tume inapendekeza:

- (i) Msamaha kwa wafungwa wa makosa yaliyotendeka katika sheria za muungano utolewe na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

baada ya mawasiliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

- (ii) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iendelee na utaratibu wa kutoa msamaha wa Rais kulingana na matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

4.2 Vikao vya Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Tume ilipokea malalamiko kutoka kwa wadau kutoka Zanzibar kuwa, Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haifanyi vikao Pemba badala yake vikao vyote vinafanyikia Unguja. Ilipendekezwa kuwa, vikao hivyo vifanyike pia Pemba.

Tume ilichambua mapendekezo hayo na kubaini kuwa, vikao vya Mahakama ya Rufani hupangwa kulingana na kalenda ya mwaka wanayojipangia ndani ya Mahakama yenyewe.

Tume inapendekeza:

Utaratibu wa kupanga vikao ndani ya Mahakama ya Rufani uendelee kutumika kwa kuzingatia kalenda yake.

4.3 Udhhibiti wa Makosa ya Rushwa na Dawa za Kulevya Zanzibar

Tume ilipokea maoni ya wadau kutoka Zanzibar kuhusu changamoto ya kushughulikia makosa tajwa kwa utaratibu wa ndani kwa kila upande wa Muungano licha ya kuwa ni makosa yanayokithiri kwa pande zote hususan makosa yanayohusu dawa za kulevya. Hivyo, ilipendekezwa kuunganisha taasisi zinazopambana na rushwa na dawa za kulevya kwa pande mbili za Muungano kuwa taasisi moja.

Tathmini ya Tume imebainisha kuwa, hapo awali kulikuwa na Sheria moja, ambayo ni Sheria Na. 9 ya mwaka 1995, ambayo ilidhibiti matumizi haramu ya dawa za kulevya kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya dawa za kulevya kwa Zanzibar kuwa tatizo

kubwa, Tanzania Zanzibar ilitunga Sheria mahususi ya kupambana na dawa za kulevya ambayo ni sheria Na. 8 mwaka 2021. Sheria hii ilianzisha Mamlaka ya Kuthibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (ZDCEA) iliyoanza kazi rasmi mwaka 2022.

Hatua hii ilisababisha suala la kupambana na dawa za kulevya kuondolewa chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi. Kwa ujumla, Mamlaka hii ina majukumu ya kukamata, kupeleleza na kupeleka mahakamani. Tume ilibaini zaidi kuwa, baada ya Jeshi la Polisi kuondolewa jukumu hilo, askari wa Jeshi la Polisi hawahusiki tena moja kwa moja kushughulikia dawa za kulevya. Aidha, pamoja na uanzishwaji wa Mamlaka lakini bado changamoto ya dawa za kulevya imeendelea kuwa kubwa.

Kuhusu masuala ya rushwa, tathmini ya Tume ilibaini kuwa, makosa ya rushwa na uhujumu uchumi kwa Zanzibar yanasimamiwa na Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ambayo ni **Sheria Na. 1 ya mwaka 2012**. Sheria hii imeanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) ambayo majukumu yake ni kuchunguza na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Hata hivyo, ilibainika zaidi kuwa, pamoja na kuwepo kwa Mamlaka tajwa, suala la kudhibiti rushwa bado ni changamoto.

Tathmini zaidi ya Tume imebaini kuwa, kuendelea kushamiri kwa makosa ya dawa za kulevya na rushwa kumesababishwa na taasisi zilizopewa majukumu ya kusimamia udhibiti wa makosa hayo kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokuwa na ofisi maeneo mengi na upungufu wa rasilimaliwatu, rasilimali fedha na vitendea kazi. Majukumu ya taasisi tajwa yanashabihiana na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa Tanzania Bara.

Tume inapendekeza:

Kwa kuzingatia kuwa masuala ya dawa za kulevya na rushwa siyo ya Muungano, taasisi zinazohusika na masuala ya rushwa (ZAECA na TAKUKURU) na dawa za kulevya (DCEA na ZDCEA) zifanye jitihada za makusudi za kuimarisha ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo kubadilishana taarifa za uhalifu. Aidha, taasisi hizo zijengewe uwezo wa rasilimaliwatu, fedha na vitendea kazi.

4.4 Ushirikiano wa Jeshi la Polisi, Kikosi cha Wanamaji na Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM)

Tume inapendekeza kuwa ushirikiano uimarishwe vilevile baina ya Jeshi la Polisi na Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo katika usimamizi wa matukio ya jinai yanayotokea baharini. Pendekezo hili linatokana na kuwa mahusiano yaliyopo baina ya vyombo hivi Tanzania Zanzibar hayana mfumo rasmi wa kitaasisi na yanategemea viongozi waliopo kuelewana tu.

4.5 Chuo cha Mafunzo

Tume inapendekeza kuwa mapendekezo ya maboresho ya Jeshi la Magereza yaliyoainishwa katika taarifa ya Tume, kama itaipendeza mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, yatumike kuboresha mifumo na utendaji wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar kadri itakavyoonekana inafaa.